MACHI 19>> Rais Samia alitimiza miaka mitatu madaraka

MIAKA MITATU YA SAMIA

TPSC yazidi kuchanja mbuga

Na MWANDISHI WETU

MIAKA mitatu ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, imekuwa na mafanikio makubwa kila sekta kutokana na mageuzi yaliyopatikana.

Rais Dk. Samia aliapishwa Machi 19, 2021 baada ya kifo cha aliyekuwa rais wa awamu ya tano, Hayati Dk. John Magufuli.

Mafanikio yaliyopatikana yamekuza huduma kwa wananchi, lengo ni kuhakikishia Watanzania wanapata huduma bora za maendeleo katika nyanja tofauti.

Moja ya taasisi hizo ni Chuo Cha Utumisi wa Umma Tanzania ambacho kimejikita katika kutoa mafunzo kwa watumishi wa umma na watumishi wa umma watarajiwa.

Taasisi hiyo inabainisha kwamba katika kutekeleza malengo yake Rais Dk. Samia, ameweka alama kubwa ya mafanikio katika Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania (TPSC).

Hali hiyo inatokana na utekelezaji wa majukumu yake kwa ufanisi ndani ya kipindi cha miaka mitatu tangu aingie madarakani .

Kaimu Mkuu wa Chuo na Mtendaji Mkuu wa Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania, Dk. Ernest Mabonesho alisema, mafanikio hayo yametokana na mazingira wezeshi, shirikishi na endelevu ya kisera, kisheria na kiutendaji ya Serikali ya awamu ya Sita chini ya uongozi madhubuti wa Rais Dk. Samia.

Dk. Mabonesho alisema, katika kipindi cha miaka mitatu ya utawala wa Rais Dk. Samia, mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na chuo kuongeza kasi ya kutoa mafunzo kwa watumishi wa umma.

Alisema kuwajengea uwezo, kuongeza ufanisi, kuimarisha utendaji kazi kuhakikisha wanatoa huduma bora kwa umma kwa kuzingatia kuzingatia weledi na matokeo chanya.

Kaimu Mkuu wa Chuo, alisema chuo katika kutekeleza majukumu yake kimeweza kuendesha mafunzo ya muda mfupi kwa watumishi wa umma 25,349 ambapo 6,684 ni mafunzo ya awali (Induction Course) kwa watumishi wa umma, 15,974 ni mafunzo ya uongozi na utawala na 2,691 ni mafunzo ya umahiri kwa watumishi wa umma.

"Mafunzo haya yamekuwa chaguo sahihi la kukuza na kuendeleza uwezo wa watumishi wa umma wa kuwahudumia wananchi katika sehemu zao za kazi" alisema.

Aliongeza; "Mafunzo haya, hasa ya awali (Induction) yametokana na ajira za watumishi wapya katika utumishi wa umma ambao wanatakiwa kupata mafunzo ya awali kabla ya kuanza kazi,"

Pia, Dk. Mabonesho alisema kwanza chuo kimeendelea kufanya tafiti tumizi, shauri za kitaalamu na utafiti ni moja ya nguzo tatu za chuo chao.

"Kwa kuzingatia umuhimu huu, chuo kupitia kitengo chake cha Utafiti na Machapisho kimefanikiwa kuratibu mradi mmoja wa tafiti unaoendelea hapa chuoni.

"Vile vile idadi ya machapisho ya watafiti wa chuo kwa mwaka 2022/23 ilikuwa ni jumla ya 12, aidha chuo kimefanya shauri za kitaalamu zipatazo 11," alisema.

Katika kutoa mafunzo kwa watumishi, Dk. Mabonesho alisema katika kipindi cha miaka mitatu ya uongozi wa Rais Dk. Samia, chuo kimepeleka watumishi mafunzo ya muda mrefu na mfupi.

Alisema lengo la kuwajengea uwezo wa kitaaluma, umahiri, stadi na weledi katika kufanikisha malengo na majukumu ya msingi yake.

> Kwa kuzingatia umuhimu huu, chuo kupitia kitengo chake cha Utafiti na Machapisho kimefanikiwa kuratibu mradi mmoja wa tafiti unaoendelea hapa chuoni.

"Hadi sasa chuo kinasomesha watumishi 19 katika mafunzo ya muda mrefu kwa ngazi tofauti za elimu, ambao watumishi watano wanasomea Shahada ya Uzamivu (PhD), saba Shahada ya Uzamili (Masters) na tisa (09) ya Shahada ya Kwanza," alisema Dk. Mabonesho.

Dk. Mabonesho alisema, kupunguza gharama za uendeshaji na kutoa huduma bora, chuo kimeanza awamu ya pili ya ujenzi wa Kampasi ya Singida katika eneo la Mungu Maji.

"Kukamilika kwa kampasi hii kutakipunguzia chuo gharama ya kulipa kodi katika majengo iliyopangwa," alisema.

Chuo Cha Utumishi wa Umma Tanzania (TPSC) ni miongoni mwa taasisi za serikali elimu ya juu nchini ambayo inatoa elimu bora sanjari na kuiunga mkono serikali katika ujenzi wa uchumi wa viwanda na ujenzi wa Tanzania mpya, Tanzania yenye neema kwa raia wake wote.

Dk. Mabonesho alisema Chuo Cha Utumishi wa Umma Tanzania kilianzishwa mwaka 2000 chini ya sheria ya wakala No.30 ya mwaka 1997 kupitia Mpango wa Uboreshaji Utumishi wa Umma (PSRP).

Dk. Mabonesho alisema chuo kimepanuka kwani idadi ya wanachuo, vitendea kazi na idadi ya kozi zimeboreshwa kwa uwiano mzuri.

Alizitaja kozi zinazotolewa na chuo hicho kuwa ni Utunzaji Kumbukumbu na Nyaraka na Uhazili.

Nyingine ni Rasilimali Watu, Utawala wa Umma, Manunuzi na Ugavi na Utwala wa Serikali za Mitaa .

Alisema chuo kinatoa mafunzo katika ngazi ya Shahada ya kwanza ikiwemo fani za Uhazili na Menejimenti ya Kumbukumbu na Nyaraka katika tawi la Dar es Salaam.

Aliongeza chuo kina matawi sita ambayo ni Dar es Salaam, Tabora Mtwara Tanga, Singida na Mbeya.

WANANCHI WATOA USHUHUDA

Juma Kapama (45) mkazi wa jijini Dar es Salaam alisema mongoni mwa taasisi zinazofanya vizuri katika kutoa mafunzo kwa watumishi wa umma ni TPSC.

"Waendelee kuwapiga msasa watumishi wa umma katika fani mbalimbali kwani kwa kufanya hivyo wanaharakisha maendeleo ya nchi yetu," alisema.

Shaka ataka c... kuwaunganish...

Na MWANDISHI WETU

MKUU wa Wilaya ya ... Shaka Hamdu Sh... dini ziendelee k... Watanzania, kuhamasish... mshikamano.

Amewasisitiza Watan... mtukufu wa Ramadhan kuv... na kuwaunganisha ku... maelewano.

Shaka ameyasema ha... wa Mkoa wa Morogoro, alipomwakilisha katika m... Qur'an yalioshirikisha wa... Morogoro, Pwani na Iringa... vya Msikiti wa Bomani jijini...

Alisema kuwa kila Mta... halina dini bali wananchi w... imani mbalimbali, hivyo k... kuabudu kulingana na Iman...

Mkuu huyo wa wilaya... kiongozi wa dini kudhani Ta... au Imani yoyote.

"Kila mtanzania nch... binadamu anayestahili hes... wa katiba yetu. Taifa letu k... wa kuabudu bila kuvunja m... kundi lenye lengo la kuvuru... chuki lilaaniwe na jamii ya w...

"Tunahitaji kumshuhudi... mbegu za amani, umoja n... Mungu tune Rais Samia mw... kubwa anaiyoifanya kutung... kuungwa mkono na kila n... maendeleo endelevu ndani...

Pia, aliwataka viongozi... ya kuipika mioyo ya waumi... na kuwaeleimisha fadhila... Munngu, kuendewlza uper... na hata wasio na dini.

Akizungumza kadhia... Mohamed Masenga, ames... serikali katika kuwaunga... ambalo nchi imeendelea k... umoja huku wakishuhudi... kuletea maendeleo ikifaniki...

Mashindano ya Qur'an r... inayofanyika kila mwaka... washiriki kutoka mikoa ya I... na kwa mwaka huu Shaka... kuwa mlezi wa mashin... walikabidhiwa zawadi mbal...

Dk. Nchim... msimamo c...

INATOKA...

wa Nchi za Misri na Korea... nchi zao nchini Tanzania, S... Komredi Kim Yong Su, mtaw... Mkazi wa Taasisi ya Friedric... Elisabeth Bollrich, juzi, Ofisi... CCM, Lumumba, jijini Dar Es...

Kwa upande wake, Bal... Balozi Dk. Nchimbi kuwa Nc... wa Rais Abd el-Fattah Sa... inaichukulia Tanzania mmo... wa karibu katika nyanja... ikizingatiwa kuwa nchi... ushirikiano katika miradi m... kwa *uchumi wa pande zote*...

Naye, Balozi Kim Yon... yake na Balozi Dk. Nchim... Kusini, chini ya Rais Kim Jon... Mkuu wa Chama cha Waf... kinachoongoza nchi hiyo, a... CCM, siku zote imekuwa ta... urafiki na uhusiano wa nch... viwili, uliowekewa msingi... Kiongozi wa Kwanza wa Kor... Sung na Baba wa Taifa, Mw...

Pia, Mkurugenzi Mkazi ... pamoja na masuala meng... Nchimbi jinsi ambavyo FES i... ambapo Katibu Mkuu hu... ushirikiano kwa masuala ye...